IVY LEAGUE CLUSTER EXAMS

Kenya Certificate of Primary Education

UTABIRI WA MWISHO

— KISWAHILI —

SEHEMU YA KWANZA: LUGHA

Oktoba 2023 - Muda: Saa 1 dakika 40

MAAGIZO KWA WATAHINIWA (SOMA MAAGIZO YAFUATAYO KWA MAKINI)

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Uksha chagua jibu lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu cha maswali.

JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:-

NAMBARI YAKO YA MTIHANI
JINA LAKO
JINA LA SHULE YAKO

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye nambari zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (Yaani nambari ya shule. Na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa katarasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.
9. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambayo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

Mfano:
Katika kijitabu cha maswali:
22. Chagua ile ambayo si siku ya juma
A. Juzi
B. Kitojo
C. Mtondo
D. Leo

Jibu sahihi ni B.
Katika karatasi ya majibu

21. [A] [B] [C] [D] 22. [A] [B] [C] [D] 23. [A] [B] [C] [D] 24. [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **22**, kisanduku herufi **B** ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

Kitabu hiki cha maswali kina kurasa 8 zilizopigwa chapa.

KCPE 2023

Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 hadi 15. Kwa kila nafasi umepewa viteuzi vinne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.

Elimu ni mojawapo ya shughuli ____1____ sana kuyakuza ___2____ ya binadamu. Elimu haipatikani shuleni tu ____3____ huwa jumla ya mafunzo ____4____ katika mazingira ____5____ tunaishi ndani. Binadamu ____6____ kwa njia chanya ____7____ atakumbatia mafunzo shuleni, katika asasi nyingine za masomo au katika asasi za masomo na ____8____ yake. Chambilecho wahenga ____9____.

1. A. inayothaminiwa
   B. zinazothaminiwa
   C. yanayothaminiwa
   D. inaothaminiwa

2. A. ufanisi B. malengo C. maadili D. mapato

3. A. ingawaje B. mbali C. mathalani D. bali

4. A. yapatikanayo B. ipatikanayo C. zipatikanazo D. yapatikanapo

5. A. yetu ambamo B. zetu ambazo C. yetu ambayo D. zetu ambavyo

6. A. anaathiriwa B. huathiriwa C. ameathiriwa D. ataathirika

7. A. yamkini B. maadamu C. ilmradi D. endapo

8. A. makazi B. jamaa C. umma D. jamii

9. A. ukiona vyaelea jua vimeundwa
   B. elimu ni taa gizani huzagaa
   C. elimu ni dafina, hupatikana vitabuni
   D. mtaka cha mvunguni sharti ainame

Serikali inajitahidi ____10____ majukumu yake kudumisha ____11____ ya upanzi wa miche ____12____ ya miti tofauti hasa ya kienyeji. Mikakati hii inafanywa ____13____ na wananchi ____14____ ambao huonyesha upendo wao kwa ____15____ taifa.

10. A. kutekeleza B. kutendekeza C. kutelekeza D. kuteketeza

11. A. azma B. shabaha C. sera D. wajibu

12. A. nyingi B. mingi C. wengi D. mengi

13. A. kila uchwao B. dhahiri shahiri C. kila uchao D. daima dawama

14. A. waaminifu B. watukufu C. wazalendo D. watiifu

15. A. kuitumikia B. kuyatumika C. kuzitumikia D. kulitumikia

Kutoka swali la 16-30 jibu kila swali kulingana na maagizo.

16. Neno mwandani lina silabi ngapi?
    A. 1
    B. 3
    C. 5
    D. 4

17. Chagua jibu ambalo lina vihusishi pekee.
    A. Halafu, tena, juu ya, kumbe
    B. Karibu na, tangu, katika, kuliko
    C. Hatimaye, baina ya, bila, ama
    D. Ili, mighairi ya, wala, kama

18. Chagua wingi wa:
    Chifu alimuua nyani mkongwe
    A. Chifu waliwaua nyani wakongwe
    B. Machifu waliwaua nyani kongwe
    C. Machifu waliyaua manyani makongwe
    D. Machifu waliwaua manyani wakongwe

19. Teua jibu sahihi.
    A. Maria angelikuja mapema angalinipata
    B. Mtahiniwa angalitia bidii angepita mitihani
    C. Asingalikuja mapema, asingalinipata
    D. Asingelinitafuta asingalinipata

20. Ni sentensi ipi ambayo inaunganisha sentensi zifuatazo ipasavyo.
    Yohana alipiga nyoka. Nyoka alikuwa kwa Mwenda.
    A. Nyoka alipigwa kwa Mwenda na Yohana
    B. Mwenda alipigiwa nyoka kwa Yohana
    C. Mwenda alipiga nyoka kwa Yohana
    D. Nyoka alipigwa na Yohana kwa Mwenda

21. Bainisha matumizi ya **'po'** katika sentensi ifuatayo.
    Aliposimama pana siafu.
    A. wakati
    B. mahali
    C. ngeli
    D. kiunganishi

22. Onyesha kundi lenye nomino katika ngeli ya **U-ZI**
    A. uteo, wayo, ndimi, mbao
    B. nguo, waya, mbao, uta
    C. ujukuti, uyoga, zizi, ubao
    D. uzi, utitiri, wayo, ukuta

23. Ni sentensi ipi iliyoakifishwa vizuri?
    A. Hoyee, nitashinda zawadi.
    B. Naam, "akasema", "nitakusaidia."
    C. Zawadi alinunua vifaa vifuatavyo: kitabu, kalamu na kifutio
    D. Je? Unamfahamu karani huyu.

24. Kanusha sentensi ifuatayo:
    Basi lililonunuliwa limeanza kusafirisha abiria.
    A. Basi lisilonunuliwa halijaanza kusafirisha abiria
    B. Basi lililonunuliwa halijaanza kusafirisha abiria
    C. Basi halikununuliwa wala halijaanza kusafirisha abiria
    D. Basi halinunuliwi wala halisafirishi abiria

25. Chagua usemi halisi ufaao wa:
    Wafula alisema kuwa angeenda nyumbani kupumzika
    A. "Nimeenda nyumbani kupumzika," Wafula alisema
    B. "Niende nyumbani kupumzika", Wafula alisema
    C. "Nitaenda nyumbani kupumzika", Wafula alisema
    D. "Nilienda nyumbani kupumzika", Wafula alisema

26. Ni jibu lipi ni mchezo wa watoto kujificha na kutafutana?
    A. Kibe
    B. Foliti
    C. Naga
    D. Maneva

27. Methali inayotoa funzo kuwa;
    Mtoto akilelewa na mlezi mbaya, huwa mbaya pia ni
    A. Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo
    B. Mtoto akibebwa hutazama kisogo cha mamaye
    C. Mtoto wa nyoka ni nyoka
    D. Mtoto mkaidi mngojee siku ya ngoma

28. Wingi wa sentensi ifuatayo ni;
    Toto lilivunja guu la gombe
    A. Matoto yalivunja maguu ya magombe
    B. Watoto walivunja maguu ya ng'ombe
    C. Matoto yalivunja mamiguu ya mang'ombe
    D. Toto yalivunja maguu ya magombe

29. Chagua jibu sahihi.
    A. Mizani ni silabi zinazofanana kati na mwisho wa mshororo
    B. Takhmisa ni shairi lenye mishororo mitatu
    C. Kina ni neno linalorudiwa katika ubeti
    D. Ukwapi ni kipande cha kwanza cha mshororo wa shairi

30. Thumni tatu kwa nambari ni
    A. $\frac{3}{5}$
    B. $\frac{3}{8}$
    C. $\frac{8}{3}$
    D. $\frac{3}{9}$

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31-40.

Tangu nipevuka na kutofautisha baya na zuri kuna jambo ambalo limenitia kiwewe. Jambo lenyewe tumelisikia likitajwa. Mwafrika ameshindwa kuuthibiti utamaduni wake. Amekuwa ng'ombe wa shemere **akijitolea mhanga** kutumiwa kwa kila njia na jiha. Ametekwa na utamaduni wa kigeni. Kwa muda mrefu amemsujudia mtu mweupe kiasi cha kumwabudu. Mila zetu ziko wapi? Haya yote tumeyatilia masikio komango na kuyafumbia macho tusiyaone. Mwacha mila chambilecho ni mtumwa. Nasi pia tumekuwa watumwa na wakimwa.

Ukichambua ndani utaona mwafrika ameiga mambo mengi sana. Tazama dini, elimu, mavazi, maadili na mengine mengi. Hebu tuliangalie jambo la lugha. Siku hizi nimepigwa na butwaa kuona kwamba lugha za mama zinafifia. Nilimwuliza banati mmoja aliyeniambia yeye ni mwafrika Mkenya ilhali hajui lugha yake ya kiasili. Anakijua Kiswahili kwa asilimia ndogo sana akikanganya kuwa ni lugha ya wale ambao hawajaelimika. Alikisifu Kiingereza, Kijerumani na Kikongo na akanieleza jinsi ambavo amebobea na kutopea katika lugha hizi.

Ndege mwigo hana mazoea na ukimwiga tembo kunya utapasuka mwaranda. Ni vizuri kuzithamini lugha zetu. Lugha ya Kiswahili ilipewa hadhi zake pindi mataifa ya Afrika mashariki yalipojinyakulia uhuru. Ni lugha ambayo ilipewa kipaumbele hata ikawa inatumika katika vikao vya bunge na sherehe maalum za Kiafrika. Pili lugha hii inazungumzwa kote Afrika mashariki hivyo basi inaunganisha jamii zetu. Tatu Kiswahili ni chombo cha kukuza ushirikiano na utangamano baina ya jamii zetu.

Serikali za mataifa yote ya Afrika mashariki yaani, Kenya, Uganda na Tanzania zina jukumu kubwa la kukiendeleza Kiswahili. Waswahili husema masikio hayapiti kichwa lakini hapa petu msemo huu umedhihirika **dhahiri shahiri**. Sisemi kuwa lugha ya Kiingereza isizungumzwe. La hasha! Lakini viongozi wa serikali zetu wakitengee Kiswahili nafasi yake ambayo kinapaswa kumiliki. Wakenya tujivunie Kiswahili. Ikiwa kuna wamarekani ambao wanafika hapa petu kujifunza Kiswahili na sisi je? Tayari idhaa ya BBC ni ngaringari kwa miaka mingi. Sauti ya Amerika haijaachwa nyuma. Kuna idhaa nyingine Ujerumani na hata pia nchini China zinazotangaza kwa Kiswahili. Je, Mwafrika haoni hayo? Heko Sheikh Shaaban Robert. Hongera mtafiti Sheikh Ahmed Nabhany. Sifa teletele zikwendee mwandishi mwenye utashi wa kuandika Ken Walibora na mwisho mshairi wa aso mtashi mwalimu Hassan Mbega. Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na karama awaweke chini ya kivuli cha amani na itifaki.

31. Kulingana na aya ya kwanza kushindwa kwa mwafrika kuuthibiti utamaduni wake ni jambo ambalo
    A. linahitaji mtu apevuke na kuelimika
    B. limesikika likitajwa kwa nadra sana
    C. si geni, limekuwa likitajwa mara nyingi
    D. limemrudisha mwafrika nyuma na kumlimbikizia uchochole

32. Maneno **akijitolea mhanga** yalivyopigiwa mstari ni fani gani ya lugha?
    A. Tashhisi
    B. Istiara
    C. Nahau
    D. Tashbihi

33. Kulingana na aya ya tatu, ni wapi hasa lugha ya Kiswahili haikutumika
    A. mijadala na vikao vya bunge
    B. sherehe za kitaifa kama jamhuri
    C. kwenye afisi ya katibu wa wizara
    D. wakati wa kuadhimisha sikukuu ya madaraka

34. Watu weupe katika kifungu wamepewa jina gani?
    A. miungu
    B. wakimwa
    C. watumwa
    D. ng'ombe wa shemere

35. Kulingana na aya ya nne
    A. Kiswahili kinatumika Afrika mashariki pekee
    B. wakenya lazima tujivunie Kiswahili na kukimiliki
    C. Kiswahili si chombo cha kukuza ushirikiano na utangamano baina ya jamii
    D. Kiswahili kinazungumzwa bara nzima la Afrika

36. Ni mataifa mangapi ambayo yametajwa katika taarifa hii
    A. 5
    B. 3
    C. 6
    D. 7

37. Katika kanda yetu ya Afrika mashariki masikio yamepita kichwa. Maana yake ni
    A. watu wameanza kuumbwa masikio yakiwa juu ya kichwa
    B. watu wameyang'oa masikio na kuyapachika vichwani pao
    C. watu wameiga tabia na nyendo za watu weupe
    D. waafrika wemekidunisha Kiswahili na kutokipa kipaumbele

38. Kulingana na kifungu hiki, ni methali ipi isiyostahili kupigia mwafrika?
    A. Vishindo vya mashua havishtui bahari
    B. Ukimwiga ndovu kunya utapasuka mwaranda
    C. mwacha mila ni mtumwa
    D. ndege mwigo hana mazoea

39. Kulingana na kifungu, ili mtu aweze kutofautisha baya na zuri inabidi
    A. aweze kuwa mtaalamu wa kutofautisha mabaya na mazuri
    B. awe amejua kutofautisha baina ya baya na zuri
    C. awe amekomaa kiasi cha kutofautisha kati ya baya na zuri
    D. awe anajua lugha zote katika bara la Afrika

40. Maana ya **dhahiri shahiri** ni
    A. bila kujulikana
    B. fiche
    C. isiyoeleweka
    D. wazi

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.

Nusura alizaliwa na kulelewa katika aila iliyojiweza, hakuwa tu mlalaheri tajika, bali pia alikuwa mtu mwenye mkono wazi aliyewapiga jeki kwa hiari wahitaji wote. Kinyume na watu wengi walio na vyao, Mzee Malimengi hakuwa mgumu wa kutoa kwani alielewa fika kuwa aliyempa kiti ndiye aliyewapa wengine kumbi. Kila siku, majirani walifululiza kwake kama maji mtoni wakiwa na hitaji moja au jingine, naye hakuwasuta. Nusura ndiye aliyekuwa mwanawe wa pekee, hivyo basi aliamua kumlea kwa inayofaa ili ajifae yeye mwenyewe maishani pamoja na jamii yake nzima. Naye alifahamu kuwa malezi bora huhitaji kujitolea mhanga. Alimsomesha mwanawe huku akimhimiza kuwa na bidii maishani kwani **bahati ni chudi**. Naye Nusura hakumuuma babake kidole. Aliyafuata mabonge ya nasaha kwa jino na ukucha. Ijapokuwa Malimengi alikuwa na mali lukuki ambayo mrithi alikuwa mwanawe tu, alimuonya dhidi ya kuegemea nundu, kwani afanyaye hivi huwa maskini.

Skulini, Nusura alikuwa mwenye nidhamu, mtiifu, mvumilivu na mnyenyekevu kwa wengi. Alijikaza kisabuni masomoni ili afue dafu. Aidha, hakujihusisha na watoto wenye tabia mbaya. Kwani alijua wazi kuwa nazi mbovu harabu ya nzima. Aliyakumbatia masomo kwa hamu kubwa, kamwe hakuwa na wakati wa kufanya **ajizi kwani babake alikuwa mkali** mithili ya simba na daima hakudekeza ugoigoi maishani. Alitaka mwanawe awe mwenye ufanisi maishani kama yeye tu. Chambilecho wahenga, mtoto akibebwa hutazama kisogo cha nina. Miaka minane ilipita ghafla. Nusura alikamilisha masomo ya shule ya msingi. Alivuna mavuno mengi kwa vile alikuwa na bidii. Alijiunga na shule tajika ya upili na wembe ukawa ni ule ule.

Hata hivyo, baada ya kumaliza kidado cha kwanza na kujiunga na kile cha pili maisha ya Nusura yalianza kuingia ufa, kitumbua chake kiliingia mchanga. Alikutana na rijali mmoja aliyeitwa Zumbukuku ambaye walilala naye bweni moja ingawa yeye alikuwa kidato cha tatu. Zumbukuku aliwarai vijana wengine shuleni kujiunga naye kutokana na tabia yake ya ucheshi na uchangamfu. Alikuwa mwepesi wa maneno na kamwe asingeweza kusemezana nawe ukose kuitikia au kuamini yale ya kumtoa nyoka pangoni. Ukweli ni kwamba, kijana Zumbukuku alikuwa mlanguzi wa dawa za kulevya humo shuleni. Aliwauzia wanafunzi wenza dawa hizo nao walikuwa wateja wake. Nacho kinolewacho hupata, Nusura akawa mteja wa Zumbukuku wa kuaminika.

Kadri siku zilivyoyoyoma ndivyo Nusura aliendelea kuwa mraibu wa dawa za kulevya, matokeo yake yalianza kudorora. Mwanafunzi aliyekuwa daima akishika hatamu za uongozi, sasa akawa nafasi hiyo hawezi hata kuikaribia tena. Iliwalazimu walimu kuchunguza chanzo cha hali hiyo. Ingawa Nusura hakuwa tayari kupasua mbarika, ukweli hatimaye ulibainika baada ya uchunguzi kufanywa. Kweli, hakuna kirefu kisichokuwa na ncha. Hali hiyo ilifichua maovu mengi yaliyokuwa yakifanywa humo shuleni. Wanafunzi walishikwa sikio na kupewa ushauri nasaha. Hatimaye walibadilika na kutia bidii wote wakapasi mtihani.

41. Kwa mujibu wa aya ya kwanza ni sahihi kusema kuwa
    A. familia aliyolelewa Nusura iliishi maisha ya bahati nasibu
    B. familia aliyozaliwa Nusura ilikuwa ya walalahoi
    C. familia aliyozaliwa na kukulia Nusura ilikuwa tajiri
    D. Nusura hakuridhika na maisha ya ukata nyumbani kwao

42. Methali **'bahati ni chudi'** imetumika kwenye taarifa. Ni methali ipi nyingine haiwezi kutumika badala yake?
    A. Mtaka cha mvunguni sharti ainame
    B. Mchumia juani hulia kivulini
    C. Mgagaa na upwa hali wali mkavu
    D. Mbio ya sakafuni huishia ukingoni

43. Zifuatazo ni sifa zinazoelezea mienendo ya Malimengi isipokuwa
    A. mkono wazi
    B. mkwasi bahili
    C. mwenye moyo mkunjufu
    C. mwenye roho ya utu

44. Nusura alizingatia ya wahenga kuwa nazi mbovu harabu ya nzima kwa
    A. kuzingatia nidhamu ya unyenyekevu
    B. kutojihusisha na wana wenye mienendo potovu
    C. kutia bidii masomoni bila kuangalia mali ya baba yake
    D. kuasi tabia ya kudekeza ugoigoi maishani

45. Kwa mujibu wa aya ya tatu kitumbua cha Nusura kiliingia mchanga
    A. kabla ya kijiunga na kidato cha kwanza
    B. wakati alipokuwa mcheshi na mchangamfu
    C. wakati alipojiunga na kidato cha pili
    D. wakati alipokataa kufuata rai ya kijana Zumbukuku

46. Kulingana na makala si sahihi kusema
    A. Mzee Malimengi alimlea mwanawe kwa kumuonyesha asali za dunia
    B. Mzee Malimengi alijifunga nira kumlea mwanawe
    C. Nusura aliyafuata vilivyo mawaidha ya babake
    D. Mzee mali mengi hakupenda mwanawe awe maskini kwa kukosa

47. Kauli, **"babake alikuwa mkali mithili ya simba"** imetumia tamathali gani ya usemi?
    A. Nahau
    B. Tashhisi
    C. Tashbihi
    D. Majazi

48. Kwa mujibu wa kifungu
    A. hatufai kujihusisha na watu wenye mali nyingi
    B. hatufai kujihusisha na watu wenye mienendo benibeni
    C. Vijana wanapaswa kuuza mihadarati nje ya shule wala sio ndani
    D. Vijana hawapaswi kujihusisha na wenzao kamwe shuleni

49. Kulingana na ufahamu **"kufanya ajisi"** inamaanisha
    A. kuwa na mzaha
    B. kuacha masomo
    C. kuwa na kichaa
    D. kukosa adabu

50. Kulingana na ufahamu, hali ya Zumbukuku kuishi bweni moja na Nusura na akaathirika inaweza elezewa na methali ipi?
    A. Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu
    B. Mtoto wa nyoka ni nyoka
    C. Baada ya dhiki ni faraja
    D. Kikulacho ki nguoni mwako